FUNZO LA 27

1. Je, huyo Farao mpya aliwafanyia nini Waisraeli?
-Farao aliwafanya Waisraeli wote kuwa watumwa.

2. Je, kwa nini Farao aliwafanya Waisraeli watumwa?
-Kwa sababu Farao alihofu kuwa Waisraeli wangetawala nchi yake.

3. Je, kwa nini Farao alihofu kuwa Waisraeli wangetawala nchi yake?
-Kwa sababu Waisraeli waliongezeka wakawa watu wengi.

4. Je, ni nani aliyekuwa akielekeza Farao kuwafanya Waisraeli watumwa?
-Shetani.

5. Je, kwa nini Shetani alitaka kuwaharibu Waisraeli?
-Kwa sababu Shetani alijua kuwa Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi kupitia kwa Waisraeli.

6. Je, kwa nini Mungu aliwabariki Waisraeli?
-Kwa sababu Mungu aliwapenda Waisraeli.
-Kwa sababu Mungu hangevunja ahadi yake kwa Abrahamu, Isaka na Yakobo.

7. Je, kwa nini Mungu alimtuma binti ya Farao kumwokoa Musa?
-Kwa sababu Mungu alipanga kuwaongoza Israeli kutoka Misri kupitia kwa Musa.



8. Je, Waisraeli wangeweza kujiokoa kutoka kwa Farao?
-La.

9. Je, Musa aliweza kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa Farao?
-La.

10. Je, ni nani pekee aliyeweza kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa Farao?
-Mungu.

11. Je, ni nani pekee awezaye kuwaokoa watu kutoka kwa Shetani?
-Mungu.

-Waisraeli waliishi Misri kwa utumwa miaka 400.

-Kwa sababu Waisraeli waliteseka sana, walimlilia Mungu.

Tusome Kutoka 2:23b

23-Wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia; kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa.

-Je, Mungu alisikia kilio cha Waisraeli?

Tusome Kutoka 2:24-25

24-Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo.

25-Mungu akawaona wana wa Israeli, na Mungu akawaangalia.

-Mungu alisikia kilio cha Israeli.

-Mungu pia alikumbuka ahadi yake kwa Ibrahamu, Isaka na Yakobo.

-Je, ahadi ya Mungu kwa Ibrahamu, Isaka na Yakobo ilikuwa ipi?

-Ahadi ya Mungu ilikuwa kwamba, baada ya miaka 400, angewarejesha Waisraeli Kanaani.

-Labda Waisraeli walidhani kuwa Mungu aliwasahau, lakini Mungu hawezi sahau.

-Mungu hufanya kile anachoahidi kufanya.

-Ijapokuwa Mungu haarakishi, yeye hutenda anachoahidi kwa wakati wake.

-Je, Musa alikuwa wapi?

-Mungu hakuwa amepanga kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri kupitia kwa Musa?

-Je, Mungu hakupanga kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri kupitia kwa Musa?



-Kwa sababu Farao alitaka kumuua Musa, Musa alitorokea nchi ya Midiani.

-Katika nchi ya Midiani, Musa alioa na akawa na wana wawili.

-Siku moja, Musa alipokuwa akilisha kondoo wa baba mkwewe, aliona mwangaza wa ajabu.

Tusome Kutoka 3:1-3

1-Basi huyo Musa alikuwa akilichunga kundi la Yethro mkwewe, kuhani wa Midiani; akaliongoza kundi nyuma ya jangwa, akafika mpaka mlima wa Mungu, hata Horebu.
2-Malaika wa Bwana akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kijiti; akatazama, na kumbe! Kile kijiti kiliwaka moto, nacho kijiti hakikuteketea.
3-Musa akasema, Nitageuka sasa, niyaone maono haya makubwa, na sababu kijiti hiki hakiteketei.

-Je, Musa aliona nini?
-Musa aliona kichaka kikiwaka moto ila hakikuharibiwa.

-Je, kwa nini kichaka kilichokuwa kikiwaka moto alichokiona Musa hakikuharibiwa?

-Kwa sababu Mungu alikuwa ndani ya hicho kichaka.

-Kwa sababu Mungu alikuwa ndani ya hicho kichaka, hakikuharibiwa.

-Mungu ni mwenye nguvu zote.

-Hakuna anayeweza kufanya kile ambacho Mungu anaweza kufanya.

-Je, kwa nini Mungu alikuwa ndani ya kichaka kilichowaka moto?

-Kwa sababu Mungu alitaka kunena na Musa kuhusu Waisraeli.

-Je, Waisraeli walikuwaje kama kichaka kilichowaka moto?

-Kama vile moto ulivyotaka kuharibu kichaka ndivyo Farao alivyojaribu kuharibu Israeli.

-Kama vile Mungu alivyokuwa ndani ya kichaka kilichowaka moto, ndivyo alivyokuwa na Waisraeli.

-Shetani na Farao hawangeweza kuwaharibu Waisraeli Mungu akiwa nao.

-Kutoka katika kichaka kilichowaka moto, Mungu alimuita Musa kwa Jina.

Tusome Kutoka 3:4

4-Bwana alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame, Mungu akamwita kutoka katikati ya kile kijiti, akasema, Musa! Musa! Akasema, Mimi hapa.



-Musa hakujua kuwa Mungu alikuwa ndani ya kichaka kilichowaka moto hadi Mungu aliponena naye.

-Je, Mungu alijuaje lugha ya Musa?

-Mungu anajua lugha zote.
-Hakuna lugha asiyojua Mungu.

-Mungu anajua lugha yako pia.
-Mungu anasikia kila kitu unachosema.
-Mungu anaelewa kila kitu unachosema.

-Hata unapononong'oneza, Mungu anasikia.

-Mungu alinena na Musa kutoka kwa kichaka kilichowaka moto:

Tusome Kutoka 3:5-6

5-Naye akasema, Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu.
6-Tena akasema, Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Musa akaficha uso wake; kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu.

-Je, kwa nini Mungu alimwambia Musa avue viatu vyake?

-Kwa sababu Musa alikuwa amesimama mbele ya Mungu mkamilifu.

-Kwa sababu Musa alisimama mbele ya Mungu mtakatifu.

-Kisha Mungu akamwambia Musa kuhusu Waisraeli.

Tusome Kutoka 3:7-10

7-Bwana akasema, Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri, nami nimekisikia kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao; maana nayajua maumivu yao;
8-nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema, kisha pana; nchi ijaayo maziwa na asali; hata mahali pa Mkanaani, na Mhiti, na Mwamori, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi.
9-Basi, tazama, kilio cha wana wa Israeli kimenifikilia; tena nimeyaona hayo mateso ambayo Wamisri wanawatesa.
10-Haya, basi, nitakutuma sasa kwa Farao, ili upate kuwatoa watu wangu, hao wana wa Israeli, katika Misri.

-Mungu alimwambia Musa kuwa alisikia vilio vya Waisraeli.

-Mungu alimwambia Musa kuwa alikuwa amemchagua Musa kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri na kutoka utumwani.

-Mungu alimwambia Musa kuwa alikuwa amemchagua Musa kuwaongoza Waisraeli kurudi Kanaani.

-Je, Musa alijibu vipi?

Tusome Kutoka 3:11



11-Musa akamwambia Mungu, Mimi ni nani, hata niende kwa Farao, nikawatoe wana wa Israeli watoke Misri?

-Musa alimwambia Mungu kuwa hakuwa na uwezo wa kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri.

-Je, kwa nini Musa alimwambia Mungu kuwa hakuwa na uwezo wa kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri?

-Kwa sababu Musa alikumbuka wakati alipojaribu kuwaongoza kutoka utumwani na akashindwa.

-Je, Mungu alimjibu vipi Musa?

Tusome Kutoka 3:12

12-Akasema, Bila shaka mimi nitakuwa pamoja nawe; na dalili ya kuwa nimekutuma ndiyo hii; utakapokuwa umekwisha kuwatoa hao watu katika Misri, mtamwabudu Mungu katika mlima huu.

-Mungu alimwambia Musa kuwa angekuwa na yeye.
-Mungu pia alimpa Musa ishara.

-Je, ishara ambayo Mungu alimpa Musa ilikuwa ipi?

-Mungu alimuahidi Musa kuwa angemrejesha katika huo mlima alipoona kichaka kilichowaka moto.

-Jina la huo mlima ni Sinai.

-Je, Musa alimjibu vipi Mungu?

Tusome Kutoka 3:13

13-Musa akamwambia Mungu, Tazama, nitakapofika kwa wana wa Israeli, na kuwaambia, Mungu wa baba zenu amenituma kwenu; nao wakaniuliza, Jina lake n'nani? Niwaambie nini?

-Musa alihofu kuwa Waisraeli hawangemwamini kama angesema kuwa Mungu ndiye aliyemtuma kuwaokoa kutoka utumwani.

-Kwa hivyo Musa alimuuliza Mungu jina lake ili aweze kuwaambia Waisraeli watakapomuuliza.

-Je, Mungu alijibu vipi?

Tusome Kutoka 3:14

14-Mungu akamwambia Musa, MIMI NIKO AMBAYE NIKO;akasema,Ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli;MIMI NIKO amenituma kwenu.

-Mungu alimwambia Musa kuwa awaambie Waisraeli kuwa "MIMI NIKO" amemtuma Musa kuwakomboa kutoka kwa utumwa.

-Je, jina "MIMI NIKO" linamaanisha nini?



-Linamaanisha kuwa Mungu hana mwanzo.
-Linamaanisha kuwa Mungu hana mwisho.

-Linamaanisha kuwa Mungu amekuwa hai wakati wote.
-Linamaanisha kuwa hakuna wakati ambapo Mungu hakuwepo.

-Pia Mungu alimwambia Musa hivi:

Tusome Kutoka 3:15-18a

15-Tena Mungu akamwambia Musa, Waambie wana wa Israeli maneno haya, Bwana, Mungu wa baba zenu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amenituma kwenu; hili ndilo jina langu hata milele, nalo ni kumbukumbu langu hata vizazi vyote.
16-Enenda, ukawakusanye wazee wa Israeli pamoja, ukawaambie, Bwana, Mungu wa baba zenu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amenitokea, akaniambia, Hakika nimewajilieni, tena nimeyaona mnayotendewa huko Misri;
17-Nami nimesema, Nitawapandisha kutoka katika mateso ya Misri na kuwaingiza katika nchi ya Mkanaani, na Mhiti, na Mwamori, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi, nchi ijaayo maziwa na asali.
18-Nao watakusikia sauti yako.

-Mungu alimwambia pia awaambie kwamba Mungu wa Ibrahamu, Isaka na Yakobo alimtuma kuwakomboa kutoka utumwani.

-Je, Farao angewaachilia Waisraeli watoke Misri?

-Hiki ndicho alichosema Mungu:

Tusome Kutoka 3:19-20

19-Nami najua ya kuwa huyo mfalme wa Misri hatawapa ruhusa mwende zenu, la, hata kwa mkono wa nguvu.
20-Nami nitaunyosha mkono wangu, na kuipiga Misri kwa ajabu zangu zote, nitakazofanya kati yake, kisha baadaye atawapa ruhusa kwenda.

-Je, Mungu alijua kuwa Farao hangewaachilia Waisraeli kutoka Misri?
-Ndiyo.

-Je, Mungu alijuaje kuwa Farao hangewaachilia Waisraeli Kutoka Misri?

-Mungu anajua kila kitu.

-Kabla hujawaza wazo, Mungu anajua hilo wazo.
-Kabla huseme neno, Mungu analijua hilo neno.

-Kabla utende jambo, Mungu anajua utakachotenda.

-Musa bado alihofu kuwa Waisraeli hawangeamini kuwa Mungu alimchagua yeye kuwaongoza kutoka Misri.

-Musa alimwambia Mungu hivi:



Tusome Kutoka 4:1

1-Musa akajibu akasema, Lakini, tazama, hawataniamini, wala hawataisikia sauti yangu; maana watasema, Bwana hakukutokea.

-Kwa sababu Musa alihofu, Mungu alimpa Musa ishara mbili awaonyeshe Israeli.

Tusome Kutoka 4:2-9

2-Bwana akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Akasema, Ni fimbo.
3-Akamwambia, Itupe chini; akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake.
4-Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; (akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake;)
5-ili kwamba wapate kusadiki ya kwamba Bwana, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amekutokea.
6-Bwana akamwambia tena, Sasa tia mkono wako kifuani mwako. Akautia mkono wake kifuani mwake; naye alipoutoa, kumbe! Mkono wake ulikuwa una ukoma, umekuwa mweupe kama theluji.
7-Akasema, Tia mkono wako kifuani mwako tena. Akautia mkono wake kifuani mwake tena, na alipoutoa kifuani mwake, kumbe! Umerudia hali ya mwili wake.
8-Basi itakuwa, wasipokusadiki, wala kuisikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili.

9-Kisha itakuwa wasipoamini hata ishara hizo mbili, wala kuisikiliza sauti yako, basi, yatwae maji ya mtoni uyamwage juu ya nchi kavu, na yale maji uyatwaayo mtoni yatakuwa damu juu ya nchi kavu.

-Je, ishara ya kwanza ambayo Mungu alimpa Musa kuonyesha kuwa alimchagua Musa kuwaongoza Israeli kutoka Misri ilikuwa ipi?

-Fimbo ya Musa iligeuka kuwa nyoka, kisha ikarejea kuwa fimbo.

-Je, ishara ya pili ya kuonyesha kuwa Mungu alimchagua Musa kuwaongoza Israeli kutoka Misri ilikuwa ipi?

-Mkono wa Musa ulishikwa na ukoma alipoutia ndani ya koti yake na ukapona alipourejesha mara ya pili.

-Hata baada ya hizi ishara mbili, Musa alihofu kuwa Isareli wangekataa kumfuata.

-Musa alimwambia Mungu hivi:

Tusome Kutoka 4:10

10-Musa akamwambia Bwana Ee Bwana, mimi si msemaji, tokea zamani, wala tokea hapo uliposema na mtumishi wako; maana mimi si mwepesi wa kusema, na ulimi wangu ni mzito.



-Musa alimwambia Mungu kuwa yeye hakujua kuzungumza vyema.

-Je, Mungu alijibu vipi?

Tusome Kutoka 4:11-12

11-Bwana akamwambia, Ni nani aliyekifanya kinywa cha mwanadamu? Au ni nani afanyaye mtu kuwa bubu au kiziwi, au mwenye kuona, au kuwa kipofu? Si mimi, Bwana?
12-Basi sasa, enenda, nami nitakuwa pamoja na kinywa chako, na kukufundisha utakalolinena.

-Je, ni nani aliyempa Musa uwezo wa kuongea?
-Mungu.

-Je, ni nani aliyekuwa na uwezo wa kumfanya Musa kuongea vizuri?
-Mungu.

-Mungu alikwa anamwambia Musa kuwa angemwezesha kuzungumza vyema.

-Ingawaje Mungu alitaka kumsaidia Musa, Musa hakutaka kuwaongoza Israeli.

-Tusome kile ambacho Musa alichomwambia Mungu:

Tusome Kutoka 4:13

13-Akasema, Ee Bwana, nakuomba, tuma kwa mkono wake huyo utakayemtuma.

-Kwa sababu Musa alihofia kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri, Mungu alikasirika naye sana.

-Lakini Mungu akaahidi kumtuma mtu kumsaidia Musa kunena na Farao.

Tusome Kutoka 4:14-17

14-Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Musa, akasema, Je! Hayuko Haruni, ndugu yako, Mlawi? Najua ya kuwa yeye aweza kusema vizuri. Pamoja na hayo, tazama, anakuja kukulaki; naye atakapokuona, atafurahi moyoni mwake.

15-Nawe utasema naye, na kuyatia maneno kinywani mwake; nami nitakuwa pamoja na kinywa chako, na pamoja na kinywa chake, na kuwafundisheni mtakayofanya.

16-Naye atakuwa msemaji wako kwa watu, hata yeye atakuwa mfano wa kinywa kwako, nawe utakuwa mfano wa Mungu kwake.

17-Nawe utatwaa fimbo hii mkononi mwako, na kwa hiyo utazifanya zile ishara.

-Je, Mungu alimtuma nani kumsaidia Musa kunena na Farao?
-Ndugu yake Musa Haruni.

-Kwa sababu Mungu aliahidi kumtuma ndugu yake Haruni amsaidie, Musa alikubali kwenda.



Tusome Kutoka 4:18 & 20

18-Basi Musa akaenda na kurejea kwa Yethro mkwewe, na kumwambia, Nipe ruhusa niende, nakusihi, niwarudie hao ndugu zangu walioko Misri, nipate kuwaona kwamba wako hai hata sasa. Yethro akamwambia Musa, Haya, nenda kwa amani.

20-Basi Musa akamchukua mkewe na wanawe, na kuwapandisha juu ya punda, naye akarudi mpaka nchi ya Misri; na Musa akaichukua ile fimbo ya Mungu mkononi mwake.

-Mungu alikuwa mvumilivu kwa Musa.

-Ingawaje Musa hakutaka kuwaongoza Israeli kutoka Misri, Mungu alikuwa amemchagua.

-Je, kwa nini Mungu alitaka kuwaokoa Israeli kutoka utumwa?

-Kwa sababu Mungu aliwapenda, hakutaka waishi katika utumwa.

-Kwa sababu Mungu alimuahidi Ibrahamu kuwa angewarejesha katika nchi ya Kanaani.

-Kwa sababu Mungu alimuahidi Ibrahamu kuwa angemtuma Mwokozi kupitia kwa Israeli.

-Katika fundisho lifuatalo, tutaona jinsi Mungu atakavyo waokoa Israeli.